

IFAHAMU stendi ya mabasi ya kisasa ya Songea

UJENZI wa kituo kikuu cha mabasi unafanyika katika eneo lenye ukubwa wa hekari **15** lilipo katika Kata ya Tanga kilomita **12** toka katikati ya Manispaa ya Songea.



Ujenzi wa kituo kikuu cha mabasi Songea, ulianza tarehe 25/03/2018 na unatarajiwa kukamilika tarehe 30/09/2019. Ujenzi unafanywa na Mkandarasi CHINA SICHUAN INTERNATIONAL CORPORATION (SIETCO) na kusimamiwa na Mhandisi Mshauri BUREAU FOR INDUSTRIAL CORPORATION (BICO) ambao ni Chuo kikuu cha Dar –es- salaam.

Mkurungenzi wa Manispaa ya Songea Tina Sekambo anasema Mradi huu unahusisha ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami nzito zinazoingia, kutoka na kuzunguka kituo cha mabasi zenyet urefu wa kilomita mbili. Upana wa barabara zinazoingia na kutoka ni mita saba na barabara zinazozunguka kituo cha mabasi ni mita 12.

Kwa mujibu wa Sekambo, Mradi huu pia unahusisha, Ujenzi wa mifereji ya barabara na Ujenzi wa eneo lenye ukubwa wa mita za mraba **17,100** la kuegesha mabasi lenye uwezo wa kuegesha mabasi **92** kwa wakati mmoja. Vilevile kutakuwa na vibanda vya abiria kusubiria mabasi (shadee) **48**.



Sekambo anasema Stendi ya mabasi ya Songea pia inahusisha Ujenzi wa eneo lenye ukubwa wa mita za mraba **1800** la kuegesha Taxi lenye uwezo wa kuegesha Taksi **60** kwa wakati mmoja,Ujenzi wa Uzio mita **900**.Ujenzi wa maduka **30** na Ujenzi wa ofisi za kukatia tiketi **20**.

“Maeneo mengine yanayohusika na mradi huu ni Ujenzi jengo la Utawala,Ujenzi wa vyoo,Ujenzi wa jengo litakalokuwa na Kituo cha Polisi na Ofisi za uhamiaji,Ujenzi wa kisima cha maji safi chenye urefu wa mita **75**,Kuweka mfumo wa maji safi na maji taka ,kuingiza umeme wa TANESCO na Kuweka Taa za sola”,anasisitiza Sekambo.

Hata hivyo anasema Mradi huu mpaka kukamilika utagharimu jumla ya shilingi **6,189,340,930**. Mpaka sasa Mkandarasi amelipwa kiasi cha Tshs **2,736,965,106.20** ikiwa ni pamoja na malipo ya awali (Advance payment). Gharama za Mhandisi mshauri ni **319,571,801.60** katika fedha hizo amelipwa Tshs **180,748,637.51**.



"Hali halisi ya utekelezaji wa mradi huu ni kwamba Mpaka sasa mradi kwa ujumla umefikia asilimia 55 ya utekelezaji ambapo Ujenzi wa eneo la kuegesha Mabasi umefikia hatua ya kuweka tabaka la kokoto(CRR), ujenzi wa jengo la Utawala, maduka ofisi za kukatia tiketi na vyoo umefikia hatua ya kupiga lipu na kuweka dari sawa na asilimia 90 ambapo kazi ya kusambaza nyaya za umeme imefikia asilimia 85", anasema.

Anazitaja Kazi ambazo hazijaanza utekelezaji ni ujenzi wa jengo la kituo cha Polisi na uhamiaji, Ujenzi wa Uzio, uwekaji wa lami nzito, ujenzi wa Mifereji, uwekaji wa taa za sola, ujenzi wa vibanda vya kupumzikia abiria (shedi), uwekaji wa vitofali vya simenti kwenye eneo la maegesho ya magari na kutengeneza eneo la bustani.

Amesistiza kuwa Ujenzi wa kituo kikuu cha Mabasi, wakati wa ujenzi umesaidia kutoa ajira kwa Wananchi 250 Kati ya hao Wataalam ni 41 na wanaobaki ni Wasaidizi mbalimbali waishio katika Kata ya Tanga na Manispaa kwa ujumla hivyo kuongeza kipato kwa Wananchi.

Hata hivyo amesema baada ya kukamilika mradi unatarajiwa kutoa ajira kwa Wananchi 396 ambapo madereva na wafanyakazi wa mabasi 306, Wauza maduka 30 Wakatisha Tiketi 60 na Wafanyabiashara ndogondogo wakiwemo mama lishe na Wamachinga.

Sekambo amebainisha kuwa Mradi huu baada ya kukamilika utaisaidia Halmashauri kuongeza bajeti ya mapato ya ndani ya mwaka 2020/2021 toka

Tshs **3,749,258,100.00** mpaka Tshs **3,958,478,100.00** sawa na ongezeko la asilimia 5.29.



Mradi huu umesaidia kuongeza thamani ya Ardhi toka **shilingi 200** kwa mita ya moja ya mraba mwaka 2016 hadi **shilingi 1200** kwa mita moja ya mraba Mwaka 2019 katika kata ya Tanga na Kata za jirani na kituo kikuu cha Mabasi. “Baada ya kukamilika mradi huu utaboresha utoaji wa huduma na utaimarisha usalama wa abiria kutokana na kuwepo kwa kituo cha Polisi na Ofisi za uhamiaji ndani ya kituo cha Mabasi”, anasema Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea.

“Hata hivyo Changamoto kubwa tunayokumbana nayo katika utekelezaji wa mradi huu ni kutopata msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT). Maombi tuliyowasilisha Wizarani kwa ajili ya kusamehewa VAT kwa mradi huu wa Serikali kuititia Mkopo nafuu toka benki Dunia lakini mpaka sasa hatujapata majibu pamoja na kwamba mradi kwa ujumla unafikia mwisho”, anasema Sekambo.

Imeandikwa na Albano Midelo

Afisa Habari Manispaa ya Songea

Aprili 12,2019